



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



Dar es Salaam, 03 Oktoba, 2022

TAARIFA KWA UMMA

KUONGEZA MUDA WA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NCHINI KWA PROGRAMU AMBAZO BADO ZINA NAFASI KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wa Elimu ya Juu nchini kuwa udahili katika awamu zote tatu kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2022/2023 umekamilika kwa mujibu wa ratiba ya udahili. Majina ya waliodahiliwa katika Awamu ya Tatu yanatangazwa na vyuo husika.

2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA

Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Tatu na wale ambao hawakuweza kuthibitisha udahili katika awamu zilizopita wanahimizwa ***kuthibitisha udahili wao katika chuo kimojawapo kuanzia leo tarehe 03 hadi 24 Oktoba, 2022*** kwa kutumia namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika.

Uthibitisho wa udahili unafanyika kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili. Orodha ya majina ya waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja imewekwa kwenye tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

3.0 KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA NNE YA UDAHILI

Baada ya kukamilika kwa awamu zote tatu za udahili, Tume imepokea maombi ya kuomba kuongezwa muda wa kutuma maombi ya udahili kutoka kwa baadhi ya waombaji ambao hawakufanikiwa kupata udahili katika awamu zilizopita na pia vyuo ambavyo bado vina nafasi vimeomba vipewe muda kuendelea kudahili. Hivyo, ***Tume imeongeza muda wa udahili kwa kufungua Awamu ya Nne na ya mwisho ya udahili inayoanza leo tarehe 03 hadi 07 Oktoba, 2022.*** Tume inasisitiza kuwa waombaji ambao hawakuweza kutuma maombi ya udahili au hawakufanikiwa kudahiliwa katika

awamu zilizopita kutokana na sababu mbalimbali, watumie fursa hii vizuri kwa kutuma kwa usahihi maombi yao ya udahili kwenye vyuo wanavyovipenda. Tume inaelekeza Taasisi zote za Elimu ya Juu nchini zinazofanya udahili wa Shahada ya Kwanza kuendelea kutangaza programu ambazo bado zina nafasi.

4.0 UTARATIBU WA UDAHILI KATIKA AWAMU YA NNE

Waombaji wa udahili na vyuo wanahimizwa kuzingatia utaratibu wa udahili kwa Awamu ya Nne kama ilivyoinishwa katika **Jedwali Na. 1**.

Jedwali Na. 1: Utaratibu wa udahili katika Awamu ya Nne kwa mwaka wa masomo 2022/2023

Na.	Tarehe	Tukio
1	03 hadi 07 Oktoba, 2022	Kutuma maombi ya udahili katika Awamu ya Nne.
2	11 hadi 12 Oktoba, 2022	Vyuo kuwasilisha Tume majina ya waliodahiliwa katika Awamu ya Nne.
3	15 Oktoba, 2022	Vyuo kutangaza majina ya waliodahiliwa katika Awamu ya Nne.
4	15 hadi 24 Oktoba, 2022	Kuthibitisha udahili kwa waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja katika Awamu ya Nne na wale walioshindwa kuthibitisha udahili wao katika awamu za udahili zilizopita.

5.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika. Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

6.0 TAHADHARI

TCU inawaasa wananchi kuepuka kupotoshwa na watu wanaojiita mawakala au washauri wanaodai wanatoa huduma ya jinsi ya kujiunga na vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini.

Imetolewa na:



Dkt. Kokuberwa Katunzi-Mollel
Kny: KATIBU MTENDAJI
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA